# Utaratibu Wa Wokovu Kulingana na Neno la Mungu

**"Hili ni jema na lampendeza Mungu Mwokozi wetu, ambaye anataka watu wote waokolewe na wapate kujua ukweli" (Timotheo wa Kwanza 2:3-4) (Union Version).**

**"Bwana hakawii kutimiza ahadi yake kama watu wengine wanavyofikiria kuwa atakawia. Yeye anasubiri kwa ajili yenu, maana hapendi hata moja wenu apotee, bali huwavuta wote wapate kutubu" (2 Petro wa Pili 3:9) (Agano jipya Kiswahili chakisasa) Mwandishi Paul Highfield November 2014. Tukafanya marekebisho  mwaka wa 2021. Wabadilishaji Wa lugha: Cosmas Lemein, Cosmas Yenko.**

**Ukitaka kufahamu lengo la vitabu hizi andikia Cosmas Lemein kwa sanduku la posta 110 Narok, Kenya. au andikia kwa Email yake cplemein@gmail.com nambari yake ya simu ni ya safaricom 0725975651. Iwapo kuna makosa kwenye vitabu hizi tafadhali umfahamishe. Ukitaka kumjulisha mwandishi ambayo ni Paul Highfield ushuhuda wako, kwa ajili ya msaada wako katika kitabu hiki, unawesa kumwandikia kwa Email yake ambayo ni prhighfield@mchsi. com. Vilevile ukumbuke kwamba tuko na Website kwa http://crm-maasai.com. Nimetumia Biblia ya Habari njema kwa watu wote union version Kimaasai tulichonacho iliyo chapishua na Bible society of Tanzania na Kenya. (Paul ama Saruni Highfield Ole Ntayia. 2021)**

# Yaliyomo


Utangulizi ........................................................................ 4
Bibilia: Vitabu vingi tofauti lakini hadithi ni moja .............. 6
Kiini cha Bibilia ni Nini? .................................................. 9
Yesu ni Nani? ................................................................... 10
Utaratibu wa Wokovu ........................................................ 14
Shida .................................................................................. 15
Shida (Njia ingine ya kuangalia shida yetu ......................... 16
Suluhisho ........................................................................... 18
  Utaratibu wa Mungu kabla hatujazaliwa ......................... 19
  Kuelewa sababu ya Yesu kuja Duniani ........................... 20
  Damu ya Yesu Kristo: Patanisho katika Kifo chake ....... 21
  Neema ya Mungu ........................................................... 22
  Imani (Faith, belief and trust) ........................................ 22
  Kupewa ama Suluhisho – Kuungama na kutubu – Jibu letu kwa neema ya Mungu ........................................... 24
  Toba ............................................................................... 26
Ubatizo (Ndani ya maji mengi) .......................................... 28
Matokeo ............................................................................. 33
Mawazo yanayohusu Mambo Magumu Yatakayo kuja baadaye .......................................................................... 35
Baraka ya kufunga ............................................................. 40

# Utangulizi

Karibu katika mafundisho haya ya Utaratibu wa Wokovu. Jukumu la Wokovu wako ni jambo la muhimu sana ambalo utalikumbana nalo katika maisha yako. Mafundisho haya yatakusaidia kukuongoza ili ujue njia ambayo Mungu alitumia kwa ajili ya Wokovu wako kupitia Yesu na vile utakavyo pokea hicho alichokufanyia.

Kwa hekima, itakuwa jambo la muhimu sana kwako kama utapitia masomo haya pamoja na mwingine aliyekuwa Mkristo kwa miaka kadhaa na ana ufahamu wa yaliyomo kwenye somo hili. Ijapokuwa, kama humpati mtu wa kukusaidia, nina imani unaweza ukajifunza wewe binafsi kwa kupitia somo hili peke yako.

Kwa ninyi mtakao tumia somo hili kuwafundisha wengine itakuwa ni vyema mjifunze aya hizi kikamilifu ili muwe na ujuzi wa kujibu maswali yatakayo wakumba. Laiti mtakumbana na maswali msioweza kujibu mara moja, omba muda wa kusoma na kufanya utafiti wa maswali na kurudisha majibu kwa wanafunzi.

Kumbuka maombi kila wakati ukiomba mwongozo, hekima na uvumilivu ukiendelea kuwafundisha wengine.

Uwe tayari kwa Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yako kama mfundishaji na pia kwa ndani ya maisha ya wale wanaofundishwa.

Na Mungu atumie mafundisho haya kuwaleta watu wengi zaidi kwa Wokovu ulio ndani ya Yesu Kristo na kuwa na makusudi na ushindi wa maisha ya sasa na ya jao.


Ni tumaini langu kwamba hao wote watakaopitia (ama watakao ongozwa kupitia) somo hili na kuweka maisha yao ndani ya Kristo watakuja kutumia kumfundisha mtu fulani na huu mpango utadumu.

Na neema pamoja na upendo wa Yesu iwe pamoja nanyi kwa kadri mnavyozidi kutafuta ili mjue njia ya Wokovu na kutoa nafsi zenu kumfuata Yesu.

Na kwa hao wote wanaongoza wengine kwa mafundisho haya, Mungu awapatie Roho wa hekima, ufunuo, ushujaa , uvumilivu na upendo kama mnavyo waongoza watu kwa upole ndani ya maji ya uzima. Vilevile ukumbuke kwamba kwa kadri watu wanavyo toa maisha yao kwa Kristo, hii inakuwa ni mwanzo tu. Wanahitaji kusonga mbele kumfuata Yesu kwa mafundisho ya undani zaidi.

# BIBILIA: VITABU VINGI TOFAUTI LAKINI HADITHI NI MOJA

## Ipo Agano la Kale na Agano Jipya, lakini hadithi ni moja na ni msalaba inayounganisha zote mbili.

| Agano la Kale | Msalaba | Agano Jipya |
|---|---|---|
| |  | |

Agano la kale liliandikwa kabla ya Yesu kuja hapa duniani. Lina husu mwanzo wa dunia, kuanguka kwa binadamu ndani ya dhambi, kuongezeka kwa maovu kwa binadamu wote, gharika kuu, Mungu alianza upya kwa Noa pamoja na familia yake, kutawanyika kwa mataifa, pamoja na kuitwa kwa Abrahamu na vizazi vyake walioitwa Israeli. Mpango wa Mungu au kazi yake ilikuwa kuwarudisha binadamu kwake. Alichagua Abrahamu kufanya hivyo kwa kumwita na kumuahidi kumbariki na kumfanya baraka kwa mataifa.

Isak alizaliwa na Abrahamu pamoja na mke wake Sara. Halafu Yakobo na Esau walizaliwa na Isak. Yakobo alikuwa na wavulana kumi na wawili, moja wao aliitwa Yosef. Yosef aliuzwa na ndungu zake kwa utumwa, lakini Mungu alikuwa pamoja na yeye na kumfanya kiongozi wa maana katika nchi ya Misri.

Baadaye ikatokea kiangazi, ndugu zake Yosef wakaenda Misri kutafuta chakula. Ndugu zake hawakumtambua Yosef siku ya kwanza, lakini aliwasamehe akajitambulisha nao.

Baada ya hayo Yosef akaondoka kwenda kuishi Misri. Lakini Yosef alipokufa Mfalme mwingine alipatikana na kutawala, akaanza kuwatesa watu wa Israeli. Watu wa Israeli wakateswa na kuingizwa utumwani katika nchi ya Misri kwa muda wa miaka mia nne (400). Ndipo Mungu akamwita Musa, akafanya kiongozi mwenye ujasiri mwingi, ili awaongoze waisraeli kuwatoa katika utumwa na kuwapeleka katika nchi ya ahadi. Wokovu wao katika nchi ya Misri ilikuwa ni mfano wa wokovu ambayo Mungu aliwapa wote waliomwamini Yesu na kumtii kwa vitendo na ukweli. Mungu aliwapa wana wa Israeli amri ya kuwaongoza na kuweka utaratibu ili Israeli iwe shahidi kwa watu wa ulimwengu mzima. Mungu alitaka mataifa wamtambue kwa upendo wake, kwa nidhamu na matunzo kwa kupitia Israeli. Vilevile aliwataka Waisraeli pamoja na mataifa yote kuona vile walivyomtaka yeye ijapo hawakuweza kuishi maisha matakatifu mbali na yeye.

Baadaye waisraeli wakawa na Waamuzi *(judges*) na Wafalme pamoja na wanabii kuwaongoza na kuwahubiria Neno la Mungu. Lakini watu walitenda dhambi, Mungu akawatumia hukumu, na nchi yao ikaharibiwa.

Lakini, Mungu akawa na mpango wa kuwarudisha katika nchi yao na kuwatumia mtumishi wake, Mesia, kwa Israeli kama taifa teule na kushiriki pamoja nao Habari Njema ya Wokovu. Kwa hiyo, wanabii wake walitangulia kutabiri siku ambayo mtumishi wake wa ahadi atakapokuja.

Siku moja Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee kwa binadamu ili aishi pamoja nao na kuwaonyesha upendo na uwezo wa Mungu. Alifundisha ya kwamba binadamu anastahili kumwamini kama Mwana wa Mungu, tubuni na mzaliwe mara ya pili. Lakini wengi wao waliona kama ni mtu anayejifanya na kuwadanganya, kwa hiyo walimkataa na

kumsulubisha. Hata hivyo, kwa uwezo wake Mungu, aliweza kufufuka na kujionyesha mbele ya watu wengi.

Baada ya hayo, akawapa wanafunzi wake Kazi kuu na kuwaamrisha waende na kuwafanya watu wa mataifa yote wawe wanafunzi wake, mkiwabatiza kwa jina la Baba, nala Mwana, na Roho Mtakatifu na kuwafundisha amri za Yesu (Matayo 28:18-20). Kazi hii ni uendelevu ya kazi ya kwanza ambayo Mungu alimpatia Abrahamu katika kitabu cha Mwanzo 12. Ndipo Yesu akarudi kwenda mbinguni na kumtuma Roho Mtakatifu kwa wafuasi wake. Wakaanza kuwahubiria wengine Habari Njema ya Yesu kwamba alikufa na kufufuka kwa ajili ya dhambi zao, alifufuka kutoka mauti, na kama watamwamini, na kutubu na kubatizwa, wataweza kupokea msamaha wa dhambi, Roho Mtakatifu, na kuwa kiungo cha kanisa lake.

Yesu aliporudi mbinguni aliahidi kurudi mara ya pili kuhukumu dunia na kuwapokea wote waliomwamini.

Sasa ni jukumu la Wakristo wote kuendeleza kazi kuu ya Mungu kwa kushirikiana Injili pamoja na wengine na kuonyesha upendo(compassion) wa Yesu kwa vitendo vya upendo na huruma.

# KIINI CHA BIBILIA NI NINI?

**1.** Kulingana na **Timoteo wa Pili 3:16 na 17** Maandiko yote Matakatifu (Bibilia) yameandikwa kwa muongozo wa Mungu aliowaongoza.

**2.** Kulingana na **Petro wa Kwanza 1:20, 21,** Unabii wa Maandiko Matakatifu hayakupatikana kutokana na Utafsiri wa nafsi wa nabii. Vilevile Unabii haujapatikana kwa msingi ya matakwa ya binadamu, lakini watu waliweza kunena kutoka kwa Mungu kama walivyoon-gozwa na Roho Mtakatifu.

**3.** Neno la Mungu linasema katika kitabu cha **Wathesalonike wa Kwaza 2:13** kwamba Neno la Mungu si kama ujumbe wa watu, bali ni neno la mungu ambalo linafanya kazi ndani yenu ninyi mnao amini.

**4.** Kulingana na **Waebrania 4:12** Neno la Mungu ni hai na lina nguvu; ni kali zaidi kuliko upanga wenye makali kuwili. Hukata kabisa mpaka mahali ambapo moyo na roho hukutana, mpaka pale vikutanapo viungo vya mwili na mafuta.neno hilo huchambua nia na fikira za mioyo ya watu.

**5. Zaburi 119:86** inasema maagizo yako yote ni amini, wananifuatia bure, unisaidiye.

**6.** Kulingana na **Zaburi 119:160** jumla yaneno lako ni kweli, na kila hukumu yako ni ya milele.

**7.** Ni wakina nani hao waliyo barikiwa kulingana na kitabu cha **Matayo 5:6?** Ni wale walio na njaa na kiu ya utakatifu.

# YESU NI NANI?

Maandiko haya yanasema nini kuhusu Yesu ni nani?

**Yohana 1.1,** *"Hapo mwanzo, kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu naye Neno alikuwa Mungu."*

**Yohana 1:14,** *"Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."*

**Yohana 4:25-26,** Aliyetamka kuwa Masihi (aitwaye Kristo).

**Yohana 5:17,** *"Akawajibu, Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi."*

**Yohana 5:18,** *"Kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivunja sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu."*

**Yohana 5:21-23,** *"Maana kama Baba awafufuavyo wafu na kuwahuisha, vivyo hivyo na Mwana awahuisha wale awatakao. Tena Baba hamhukumu mtu ye yote; bali amempa Mwana hukumu yote ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyemtuma."*

(Ijapo Yesu anazungumza kwa nafsi ya tatu ya mtu katika kitabu cha Yohana 5:21-23, ni wazi kwamba kwa mazungumzo haya anajihusisha nafsi yake anapozungumza kuhusu Mwana.)

**Yohana 5:37 -** Yesu alisema kwamba Baba aliyenituma hunishuhudia.

**Yohana 6:40,** Yesu alisema, *"Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho."*

**Yohana 6:48,** Yesu alisema, *"Mimi ndimi chakula cha uzima."*

**Yohana 7:17,** Yesu alisema, *"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu."*

**Yohana 8:31, 32,** *"Basi, Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, 'Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru."*

**Yohana 8:58,** *"Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko."*

Kwa hiyo, hii inaonyesha kwamba alikuwepo na ako hai na aliishi hata kabla hajaja duniani.

**Yohana 10:9,** Yesu akasema, *"Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka; ataingia na kutoka, naye atapata malisho."*

**Yohana 10:14, 15,** Yesu akasema, *"Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo."*

**Yohana 10:30,** Yesu akasema, *"Mimi na Baba tu umoja (pamoja)."*

**Yohana 10:36b,** Yesu akasema, *"Kwa nini basi mnanishtaki kwa kusema nimefukuru (blaspheme) kwa sababu nimesema, mimi ni Mwana wa Mungu?"*

**Yohan 11:25,** *"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi huo ufufuo, naa uzima. Yeye aniaminiye mimi hata kama atakufa, ataishi.' "*

**Yohana 12:44-46,** *"Naye Yesu akapaza sauti, akasema, Yeye aniaminyie mimi, haniamini mimi bali yeye aliyenituma. Naye anitazamaye mimi amtazama yeye aliyenituma. Mimi nimekuja ili niwe nuru ya ulimwengu, ili kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani."*

**Yohana 14:6,** *"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."*

**Yohana 15:5,** Yesu akasema, *"Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote."*

**Yohana 18:36,** Kwa kumjibu Pilato, *"Yesu akamjibu, 'Ufalme wangu si wa ulimwengu huu. Kama ufalme wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania nisije nikatiwa mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu sio wa hapa.' "*

Kwa kumjibu Pilato, *"Yesu akamwambia, 'Ufalme wangu si wa ulimwengu huu. Kama ingekuwa ya ulimwengu huu, watumishi wangu wangenipigania nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini ufalme wangu ni wa mahali pengine.' "*

**Yohana 18:37,** *"Basi Pilato akamwambia, Wewe u mfalme basi? Yesu akajibu, Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme.*

*Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni, ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli hunisikia sauti yangu."*


**Yohana 19:7,** Yohana akasema yaliyozungumzwa na wayahudi kuhusu Yesu, *"Wayahudi wakamjibu, Sisi tunayo sharia, na kwa sharia hiyo amestahili kufa, kwa sababu alijifanya kuwa Mwana wa Mungu."*

**Kwa hiyo, kwa maneno yako mwenyewe, unafikiri Yesu ni nani kulingana na maandiko haya yote?**

**Kulingangana na Matayo 16:16 na Wakolosai 1:15, Yesu ni nani?**

# UTARATIBU WA WOKOVU

**Shida**
"Mshahara wa dhambi ni mauti…" (Warumi 6:23a).



# Shida

## Ni vipi haya maandiko yanafafanua shida tuliyonayo nche ya Kristo?

Yohana 3:19, 20

Warumi 3:10

Warumi 3:23

Warumi 5:6a

Warumi 5:10a

Warumi 6:16

Warumi 6:23

Waefeso 2:1, 2

Waefeso 2:11, 12

Wakolosai 1:21

Isaya 59:2

Isaya 64:6

Yeremia 2:13

Yeremia 17:9

Wahebrania 9:27- Kulingana na mstari huu ni lazima watu wote wafe na kusimama mbele ya hukumu.

## Shida - Njia nyingine ya kutazama shida yetu.

Uliwahi kusema uongo?

Uliwahi kumtamani mtu?

Uliwahi kuiba chochote?

Uliwahi kumwabudu kitu chochote kisochokuwa Mungu wa ukweli?

Uliwahi kutaja jina la Mungu wako bure au kusema neno la kulaani?

Uliwahi kuwa na chuki ndani ya moyo wako kwa mtu mwingine?

Uliwahi kumjibu baba au mama yako vibaya?

Uliwahi kumsingizia mtu mwimgine uongo?

Uliwahi kutamani kuchukua kitu alichonacho mtu mwingine?

Kama uliwahi kufanya mojawapo ya maneno haya, umetenda dhambi na unahitaji Mkombozi. Huenda huja tenda hayo yote, lakini inawezekana umetenda baadhi yao. Bibilia inasema ya kwamba wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu (Warumi 3:23). Vivile angalia Warumi 5:20 na Wagalatia 3:19-25.

Tu wanyonge.

Tu wasinzi.

Tu maadui wa Mungu.


Tupo katika giza.

Hatuwezi kujiokoa wenyewe.

Tufanye nini?

# Tulichopewa ama Suluhisho

**Msalaba/damu ya Kristo**
**Warumi 5: 9; Petro wa Kwanza 1:18-19**
**"Zawadi kutoka kwa Mungu" – Warumi 6:23b**



# Kupewa ama Suluhisho

## Utaratibu wa Mungu kabla hatujazaliwa.

**1**. Mungu aliumba kila kitu vizuri, lakini alimpatia binadamu:

Amri ---- Mwanzo 2:16.

Uhuru wakuchagua ---- Mwanzo 3:6.

Majibu ---- Mwanzo 3:16-19.

**2**. Binadamu alichagua kutenda dhambi kwa kusema hapana kwa njia ya Mungu (Mwanzo 3:6,7).

**3**. Matokeo ni kwamba dhambi iliingia duniani (Warumi 5:12).

**4**. Mungu akawa na utaratibu wa kumrudisha binadamu kwake.

Mungu akamwita mtu aliyeitwa Abrahamu. Akamwahidi kumbariki pamoja na wajukuu wake walioitwa Waisraeli. Ndani yao wakapatikana waamuzi, Wafalme, wanabii, mwishowe akazaliwa Mwokozi, Yesu, aliye Kristo, Mwana wa Mungu.

Aliishi, akafa na kufufuka kutoka mauti ili atuweke huru, kutusamehe na kuturudisha katika ushirika wa Mungu (Mwanzo 12:1-3; Matayo 1:1-25).

**5.** Yohana 3:16 inasema nini kuhusu mpango wa Mungu?

**6**. Katika Warumi 5:6-8 Bibilia inasema kwamba Yesu alikuja kwa wakati unaofaa tulipokuwa wanyonge. Wakati tulipokuwa kafiri Kristo akafa kwa ajili yetu. Yesu alikufa kwa ajili yetu hata kabla hatujazaliwa; wakati huo tulikuwa wanyonge kabisa. Hii ilikuwa ni tendo la neema kamili kwake kutuokoa.

## Kupewa ama Suluhisho—Kuelewa kwanini Yesu alikuja duniani.

Kulingana na maandiko haya, kwa nini Yesu alikuja duniani?

**1**. Marko. 10: 45

**2**. Luka 4:18,19

(Mwaka wa "neema ya Mungu" uliitwa Jubilee. Huu ni wakati ambao madeni yalisamehewa, mashamba yalirudishwa kwa wenyewe wa mwanzo na watumwa wakaachiliwa huru. Hapa Yesu alitumia hayo maneno kwa njia ya kiroho kumaanisha msamaha na mwanzo mpya.)

**3**. Yohana 1:10-13

**4**. Yohana 1: 18

**5**. Yohana 1:29

**6**. Yohana 3:17

**7**. Yohana 9:39

**8**. Yesu hakuja ulimwenguni kwa ajili ya kufa tu, bali pia alikuja kufufuliwa kwa maisha kwa ajili ya kudhibitisha ufufuo (Warumi 4:25).

**9**. Bila ufufuko wa Yesu mahubiri yetu hayafai na imani yetu ni bure na imani yetu haitakuwa na maana hii ni kulingana na Wakorintho wa Kwanza 15: 14,17.

**10.** Wakorintho wa Pili 5:17.

**11.** Wakorintho wa Pili 5: 21.

## Kupewa ama suluhisho – Damu ya Yesu Kristo, Upatanisho kupitia kifo chake

**1.** Kwa damu ya Yesu tumeweza kudhibitishwa na kuokolewa kutokana na hasira kali ya Mungu hii ni kulingana na Warumi 5:9.

**2.** Kulingana na Warumi 5: 9-10b tumepatanishwa na Mungu kupitia kifo cha mwana wake. Na kama tumepatanishwa pia tutaokolewa kupitia maisha yake.

**3.** Ni kitu gani kilichotuokoa katika maisha yetu yasiofaa kulingana na Petro wa Kwanza 1:17-19? Jibu – damu ya dhamana ya Kristo.

**4.** Kulingana na Warumi 3:25 tunahitaji kuwa na imani katika damu ya Yesu Kristo.

**5.** Tupo na vitu gani kupitia kwa damu ya Yesu kulingana na Waefeso 1:7? Jibu - Kukombolewa kwa msamaha wa dhambi.

## Kupewa ama Suluhisho - Neema ya Mungu

**1.** Kwa sababu ya neema ya Mungu, alitumia Roho wake mtakatifu kutuelekeza njia ya imani. Yohana Mtakatifu 16:8 anasema nini kuhusu jambo hili? Roho mtakatifu atakapokuja atahakikishia dunia makosa kulingana na thambi na uadilifu na hukumu ya Mungu.

**2.** Watu waliomsulubisha Yesu waliposikia ukweli, Matendo ya Mitume 2:37 inasema wakawa walichomwa ndani ya miyoyo yao. Unafikiri ni nani alikuwa akifanya kazi ndani ya miyoyo yao kuwajulisha juu ya dhambi hii? Ni roho mtakatifu.

**3.** Warumi 3:22-24 inasema tumekubaliwa huru kwa neema ya Mungu.

**4.** Kulingana na Waefeso 2:8,9 tumekombolewa kwa njia ya imani kupitia neema lakini si kwa vitendo yenu ili asipatikane atakayejivunia kitu.

## Kupewa ama Suluhisho – Imani, Amini na tumaini wito Wetu kwa neema ya Mungu

Tunastahili tuamini Maandiko Takatifu tuliyojifunza.

Yanasema:

Sisi ni wenye dhambi.

Tupo na shida.

Tunahitaji mkombozi.

Kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu.

Kwamba alifufuka kutoka kwa mauti kwa ajili ya uadilifu wetu.

Kwamba tutakuwa na wokovu kwa damu yake kwa neema ya Mungu.

Kwamba tutakufa na kuhukumiwa.

**1.** Waebrania 11:1 inasema, *"Sasa imani ni kuwa na hakika kabisa ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana."*

**2.** Waebrania 11:6 inasema ya kwamba tusipokuwa na imani, hatutaweza kumpendeza Mungu.

**3.** Yesu alisema katikaYohana 5:24 kwamba tukiwa na imani ndani yake, tutakuwa na kitu gani? Maisha ya milele.

**4.** Warumi 3:21- 22 inasema kwamba tumefanywa waadilifu mbele ya Mungu kwa imani.

**5.** Wagalatia 3:26-29, Paulo anaunganisha imani na nini? Ubatizo.

**6.** Kama imani yetu haitakuwa na wito wa vitendo itakuwa imekufa hii ni kulingana na Yakobo 2:17, 26.

Kuna njia nne za kutazama katika Imani ya kweli: Kuelewa, kukubali na Tumaini, naa majibu yenye vitendo.(Hii ni kusikia na kutenda). Imani ni kuelewa ukweli kuhusu Yesu naa Wokovu, kukubali kwamba ni kweli naa kuamini kwamba Yesu ni Bwana na mwokozi. Imani ya kweli pia inajuimuisha majbu ya vitendo. Kwa maneno mengine kwa tafsiri ya Imani inajuimuisha toba na ubatizo na kutoa maisha yako kikamilifu

kwa Yesu naa kumfuata yeye bila kujali matatizo yatakayo tokea.

Imani ni kama mfereji au mtaro ambayo inatumika kwa wokovu wetu. Hii imani ni lazima iwe na vitendo, utiifu, hai na inazaa matunda. (Warumi 1:5 ; 10: 16; 16: 26; Waebrania 5:9 ; Yakobo 2: 24; Matendo ya mitume 6:7; 2 Wathesalonike 1: 8; Petro wa kwanza 4: 17). Kuwa na imani ya ukweli haimaanishi hutakuwa na wasiwasi tena. Lakini ukumbuke kila wakati wasiwasi wako ikuongoze kukuelekeza kwa Mungu na sio kukutenganisha naye.

## Kupewa ama Suluhisho – Kuungama na Kutubu – Jibu letu kwa neema ya Mungu

Kuungama ina sehemu mbili: Kuungama kwa dhambi na kuungama kwamba Yesu ni Bwana.

### Kuungama Dhambi

**1.** Kulingana na Nehemia 9: 1-3, watu wa Israeli walifanya nini kwa sababu ya dhambi zao? Walitubu dhambi zao.

**2.** Mwandishi wa Zaburi 32: 5 inawezekana kuwa ni Daudi kwa vile alijisikia kuhakikishiwa kwa dhambi yake ya usherati. Daudi akasema,siwezi kuficha maovu yangu. Akasema kwamba atatubu maovu yake kwa Bwana.

**3.** Katika Zaburi 38: 18 Daudi alisema, *"Nitaungama maovu yangu; nimetatizwa na dhambi yangu."*

**4.** Watu walioitikia ujumbe wa ubatizo wa Yohana Mbatizaji ni mfano mzuri sana wa wale walioungama dhambi zao.

Marko 1:5 inasema kwamba watu wote walijitokeza wakamweendea kutubu dhambi zao.

**5.** Bibilia inasema wazi kwamba imani peke yake haitoshi. Mfano mzuri wa msemo huu inapatikana kwa Yohana 12: 42. Kwa nini hawa viongozi hawataki kutubu dhambi zao? Kwa sababu ya uoga wao.

**6.** Matendo ya Mitume 19: 18 yanasema wazi kwamba Waefeso wengi walitubu matendo yao maovu.

## Kuungama kwamba Yesu ni Bwana

**1.** Yesu Mwenyewe anasema, kwa Matayo 10: 32-33, ya kwamba ni lazima mtu kukiri Yesu mbele ya binadamu.

**2.** Kulingana na Warumi 10: 9, 10 ni nini tutatubu kwa vinywa vyetu: kwamba Yesu ni bwana. (Kumbuka: Baadhi ya watu walitumia aya hii kusema kwamba yote watakayofanya, moja ni kutubu na kuamini ili waokolewe. Ijapokuwa, katika kanisa ya kwanza walitumia ungamo huu wakati wa ubatizo kuonyesha ya kwamba ungamo na ubatizo huenda pamoja kwa njia ya wokovu. Pia, Paulo anasema wazi katika Warumi 6: 1-3 kwamba tunabatizwa **ndani** ya Kristo.)

**3.** Katika Wakolosai 2: 6 Paulo anasema ya kwamba walimpokea Yesu kama Bwana.

**4**. Katika  1 Timoteo 6:12 Paulo alimfariji ndugu yake Timoteo ashikilie tuzo la uzima wa milele aliloitiwa wakati alipokiri mbele ya mashahidi wengi.

(Hii inaonyesha kwamba maungamo inaweza kuwa zoezi la mara kwa mara wakati wa Agano Jipya. Wakati mtu mmoja

anapokuwa tayari kutoa maisha yake kwa Kristo ataungama na kubatizwa mbele ya washahidi.)

**5**. Kulingana na 2 Timoteo :19, wote watakao ungama ni lazima pia waachane na dhambi.

**6.** Kwa  Matendo ya Mitume 19:18, 19, watu waachane na matendo yao maovu. Hii iliwaongoza kukusanya vitabu vyao mbele ya halaiki. Hii inadhihirisha kwamba muungamo wa kweli huelekeza watu kwa toba, ambayo ni ukamilifu wa kuachana kabisa na maisha ya zamani na kumgeukia Mungu na maisha mapya.

## Toba

Toba ni kukataa kabisa dhambi zako na dhambi ya maisha ya zamani, na kumgeukia Mungu.

**1.**Ufunuo 9:20, 21 - Yohana anazungumza kuhusu baadhi ya watu ambao hawajatubu. Kama anavyoongea juu ya toba, anazungumza akilenga dhambi ambao wamekataa kutubu. Haya ni matendo ya kukataa kutubu. Toba sio hali ya mawazo tu, bali ni kutengana na dhambi.

**2.** Siku ile kanisa ilipoanza Jerusalemu (A. D 33), Petro, mmojawapo wa wafuasi wa Yesu, alisimama na kuhubiri kwa baadhi ya mamia ya watu. Alihubiri vile Yesu alikufa kulingana na utaratibu wa Mungu na pia vile Mungu alivyomfufua kutoka kwa wafu na kumfanya Bwana.  Vilevile aliwaambia walimsulubisha Yesu bila ufahamu. Waliposikia haya, wakawa wamehakikishiwa na wakamuuliza Petro tufanye vipi ili tupate kuokolewa. Kulingana na Matendo ya Mitume 2:38, jibu la Petro lilikuwa lipi? Ni lazima mtubu na kubatizwa kwa jina la Yesu kwa msamaha wa dhambi.

**3.** Kulingana na Matendo ya Mitume 3:19, mmoja atakapo tubu dhambi humgeukia Mungu.

**4.** Paulo katika Matendo ya Mitume 20:21 alisema kwamba ni lazima watu wamgeukie Mungu kwa kutubu na kuwa na Imani ndani ya Bwana wetu Yesu Kristo.

**5.** Kulingana na Luka13: 1-3, Yesu aliwaambia watu kwamba wataangamia ama sivyo watubu.

**6.** Tunaweza kupanua maana ya toba kwa kuongea juu ya mahitaji nane ya kweli ya toba:

(1) Kutambua dhambi (kukubali) - (Luka 15:11-32; 2 Wakorintho 4:4; Matendo ya Mitume26:17, 18; Warumi 3:22,23).
(2) Huzuni ya dhambi (Zaburi 38:8,9; Luka 7:36-50; 2 Wakorintho.7:8-13; Matayo 26:75).
(3) Kukiri dhambi (Nehemia 9:13; 2 Samueli. 12: 13; 24: 10; Luka. 15:18, 1; Zaburi. 38: 18; 1Yohana 1:9, 10: Matendo ya Mitume 19:18).
(4) Aibu kwa sababu ya dhambi (Esra 9:6; Luka 7:36-38; 15:21).
(5) Chuki ya dhambi (Zaburi 97:10; 119:104, 163; Medhali. 8:13; Mhubiri 3:8; Amosi 5:15; Yohana 2:15).
(6) Kugeuka kuachana dhambi (Esekieli 13:20; 14: 6; 33: 10, 11; Isaya. 55: 7; Matendo ya Mitume 3: 26; 20:21; Ufunuo. 9:20, 21; 1Petro. 3: 10, 11; Matayo 5: 23).
(7) Huzaa matunda ya toba (Matendo ya Mitume 2:38; Luka 3:7-9; 1-10; Matendo ya Mitume 26:19, 20; Matayo. 7: 21; Warumi 12: 9).

(8) Kumkubali Yesu kama bwana wa maisha yako (Matendo ya Mitume 19:18, 19; Wakolosai. 2:6; Matendo ya Mitume 3: 19; 1Petro. 3: 15; Wafilipi 2:9-10).

## Kupewa au Suluhisho – Jibu Letu kwa Neema ya Mungu ndani ya Ubatizo (Ndani ya maji mengi)

**1.** Yohana 3: 5, Yesu alimwambia mtu aitwaye kwa jina Nikodemo kwamba, *"Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu."*

**2.** Kulingana na Matendo ya Mitume 2:38, Petro aliwaambia watu, *"Tubuni dhambi, kila moja wenu kwa jina la Yesu kristo , mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokeya kipawa cha roho mtakatifu."*

**4**. Kwa Warumi 6:1-7, Tunaweza kuona ya kwamba kupitia ubatizo tunaweza kujitambulisha kwa kifo na ufufuko wa Yesu Kristo.

Katika mstari wa tatu, Paulo anasema ya kwamba tunapobatizwa ndani ya Kristo Yesu, tumebatizwa katika kifo chake.

Mstari wa nne inasema ya kwamba tulizikwa pamoja na Yesu. Hii inafanyika kwa njia gani? Kupitia ubatizo.


Kulingana na mstari wa tano, maana, kama sisi tumeungana naye katika kifo chake, vivyo hivyo ni dhahiri kwamba tutaungana katika kufufuka kwake.

Nafsi yetu ya zamani imesulubiwa pamoja na Yesu *"Ili kwamba mwili wa dhambi iweze kuharibiwa, halafu tusirudi tena watumwa wa dhambi"* (mstari wa sita).

Mstari wa saba inasema ya kwamba kama tumekufa pamoja na Yesu, tumenasuliwa kutokana na nguvu ya dhambi.

**5.** Kwa **1 Petro 3:21,** Petro anasema ya kwamba
Na haya maji ni kama maji ya ubatizo ambayo inawaokowa ninyi sasa.Ubatizo sii shauri la kondoa uchafu mwilini bali ni dhamiri ya kumlilia Mungu kwa roho safi. Itawaokoeni ninyi kwa ufufuko wa Yesu Kristo.

**6.** Kulingana na **Wagalatia 3: 26-29**, ni wakati gani Paulo alisema "tumevalishwa" Kristo? Wakati tutakapobatizwa.




**Kusudi la ubatizo kulingana na neno la Mungu:**

1. Kwa hiyo tunaweza kufuata njia ya kristo. Yesu Matayo 3:13-17.
2. Kwa hiyo tunaweza kufuata vile Yesu alivyotuamrisha. Matayo 28: 18-20.
3. Kwa hiyo tunaweza kupokea msamaha wa dhambi. Matendo ya Mitume 2:38; 22:16.

4. Kwa hiyo tunaweza kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Matendo ya Mitume 2: 38; 1 Wakorintho 12:13.
5. Kwa hiyo tunaweza kutambulishwa na Yesu katika kifo chake na ufufuko wake. Warumi 6:1-4.
6. Kwa hiyo tunaweza kuwa kiungo cha mwili wa Kristo. (1Wakorintho 12:13; Waebrania 10:19-25). (Vile vile angalia Matendo ya Mitume 2:47 ambayo inasema kwamba "Bwana akazidisha kanisa idadi yao kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.")
7. Kwa hiyo tunaweza kuvalishwa pamoja na Kristo. (Wagalatia 3:26-29).
8. Kwa hiyo tunaweza kuachana na nafsi yetu ya zamani na kuwa viumbe vipya (2 Wakorintho 5:16-17.)
9. Kwa hiyo kiroho tunaweza kutahiriwa. (Wakolosai 2: 11, 12.)
10. Kwa hiyo tunaweza kupokea wokovu. (1 Petro 3: 21-22. (vile vile angalia Marko 16:16.)
11. Kwa hiyo tunaweza kuzaliwa tena mara ya pili kwa maji na roho.Yohana 3:5. (Neno linalotumika kwa *"tena"* linaweza pia kumaanisha kutoka "juu" Kwa hiyo, mmoja amezaliwa tena kutoka juu kwa sababu imetoka kwa Mungu.)
12. Kwa hiyo , Mungu anaweza kutufanya wapya kupitia utakazo wa kuzaliwa upya na kuwa na maisha mapya ya Roho Mtakatifu (Tito 3:4-7).

## Mambo mengine mawili yanayostahili kutuzamwa kuhusu Ubatizo

**1. Kinachofanyika katika ubatizo ni kitendo cha Mungu wala sio cha binadamu** - Kama vile tunavyotazama wazi katika Wakolosai 2: 11-13. Kumbuka kwamba Paulo anasema tohara ya kiroho haijafanyika "kwa mikono ya binadamu," bali

kwa kristo. mstari: 11b. Vile vile anasema imani yetu ipo ndani ya nguvu ya Mungu - mstari 12b.

**2. Sehemu nne muhimu ya ubatizo katika Bibilia:**


*** Njia bora utakayo tumia:** kuzama ndani ya maji – (Warumi 6:3; Wakolosai 2:12).

*** Uwezo unao stahili:** Kwa jina la Kristo (Matendo ya Mitume 2: 38; 19: 5) au kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu kama ilivyo katika Matayo 28:19,20.

*** Kusudi linalostahili:** binadamu wapate msamaha wa dhami (Matendo ya Mitume 2:38; 22:16). Lakini kuna makusudi mengine zaidi ya moja, kama tulivyoyaona mbeleni tulipozungumza tofauti kumi na mbili ya maneno takatifu kuhusu ubatizo.

*** Mtu anayehusika:** Mtu aliyetubu kikamilifu (aliyekiri dhambi) mwamini (Matendo ya Mitume 2: 38; 8: 37; Marko 16: 16; Yohana 3:16; Luka 13:1-5; Wakolosai 2:12; Petro wa Pili 3:9).

# Tulichopewa ama Suluhisho



## Matokeo

**1.** Kulingana na Warumi 5:1-2, tutakuwa na nini kwa sababu Mungu ametufanya waadilifu kwa imani? Tutakuwa na amani.

**2.** Tunapokuwa ndani ya Kristo, tumewekwa huru kutokana na dhambi na watumwa wa haki ( Warumi 6: 17-18.)

**3.** Nini jibu la kuwa ndani ya Kristo kulingana na Warumi 6: 23?   Uzima wa milele.

**4.** Katika Warumi 8: 1-2 Paulo anatuambia kwamba kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu  hawatakuwepo katika hukumu.

**5.** Kulingana na Waefeso 1: 7-8 - Ni vitu gani viwili tutakuwa nayo ndani ya Kristo? Wokovu na msamaha.

**6.** Ijapo tupo ndani ya Kristo, hatutakuwa wageni tena na wala sii watu wa nje, lakini ninyi ni raia pamoja na wateule wa Mungu. (Waefeso 2:19).

**7.** Kulingana na **1 Petro 1; 3-5**, Baraka zetu ni zipi ndani ya Kristo?

Uzao mpya
Tumaini hai
Urirthi usiyo haribika milele,usiyo na uchafu wala kufifia. Tumelindwa na nguvu mpaka wokovu utakapokuja ambayo tayari kufunuliwa mwishoni mwa nyakati.

**8.** Kwa kuwahutubia Wakristo, 1 Yohana 1: 9, Yohana anasema kwamba tukiungama dhambi zetu , basi

Mungu ni mwaminifu na mwadilifu na ametusamehe dhambi zetu, na kututakasa kwa uovu wote.

**9.** Katika 1Yohana 5:13, Yohana anasema ya kwamba, tukiamini kwa jina la Mwana wa Mungu tutajua kwamba tunayo uzima wa milele.

**10.** Kulingana na Matendo ya Mitume 2: 38, ni Baraka zipi mbili ambayo tutapokea tunapo tubu dhambi zetu na kubatizwa? Msamaha wa dhambi na roho mtakatifu

# Mawazo ya mambo magumu yanayokuja
***(Counting the cost)***

Sasa, umeshajua jinsi ya kuwa Mkristo, unahitaji kufikiria kwanza juu ya mambo magumu yanayo kuja kabla hujakata shauri. Kuna mistari nyingi katika Bibilia yanayotuambia kuhusu haya.

**1.** Sehemu ya kufikiria juu ya mambo magumu yanayokuja ni kuelewa kwamba mateso yatakuja unaposhikilia imani na wito wako.

Paulo anatukumbusha ya kwamba tutateseka katika Wafilipi 1:29, *"Maana ninyi mmepewa fadhili ya kumtumkia Kristo si tu kwa kumwamini bali pia kwa kuteseka kwa ajili yake."* (Version: Habari njema kwa watu wote.)

**2**. Ujitayarishe unapokuwa Mkristo kupokea mateso, kwa sababu hakika yatatokea.

Ujitayarishe ili usianguke katika imani. ( Soma Marko 4: 17 ili upate jibu.)

**3.** Katika Wagalatia 6:12, Paulo anaongea kuhusu hao wote wanaotafuta kuepuka mateso kwa kutafuta kuwa wazuri kwa watu fulani. *"Kwa wale wanaotaka kuonekana wazuri kwa mambo ya mwili ndio wanaotaka kuwalazimisha ninyi mtahiriwe. Wanafanya hivyo kwa sababu ya jambo moja tu: Kusudi wao wenyewe wasije kusulubiwa kwa sababu ya msalaba wa Kristo."* (Habari njema)

**4.** Katika 1 Petro 3:13-18 Petro anatufundisha jinsi tutakavyo jitayarisha ili mateso yatakapokuja yatupate tukiwa tayari. Mara ya kwanza alisema katika mstari wa kumi na nne

kwamba lasima tusiogope kitu wanacho ogopa. Kitu cha kwanza kinachotushinda kawaida ni uoga. Tunaogopa watu kwa sababu tunafikiria kwamba wanaweza kutucheka au kututesa kwa njia hii ama nyingine.

**5.** Petro akaendelea kutufundisha vile tutaweza kushinda wote watakao tutesa. Katika 1 Petro 3:15a akasema kwamba, *"Lakini mtukuzeni Kristo kama Bwana mioyoni mwenu."* Kama Yesu ni Bwana wa mioyo yetu, ni kitu gani itatufanya tuwaogope wengine? Je unamtamani Yesu kuwa Bwana wa moyo wako? (Habari Njema)

**6.** Petro anatufundisha njia nyingine itakayotuwezesha kuwa tayari katika mateso. Anatupa moyo anaposema, *"Muwe tayari kumjibu yeyote atakayewaulizeni juu ya matumaini yaliyo ndani yenu. Lakini fanyeni hivyo kwa upole na heshima.."* (1 Petro 3:15b). (Habari njema)

Petro anaendelea kusema kwamba, *"...Muwe na dhamiri njema, kusudi mnapotukanua, na wale wanaosema mabaya juu ya mwenendo wenu mwema kama Wakristo, waone aibu"* (3:16). (Habari njema)

Tunahitaji kulinda mioyo yetu tunapo ongea pamoja na wengine na kujibu maswali yao kwa makini ili wasiseme jambo lolote mbaya kutuhusu. Huenda wakati utakuja ambapo mambo yatageuka na Mungu akafanya kazi yake kwa njia isiyoaminika.

Tunahitaji kuwa tayari katika majibu ili tusibabaike na kuchanganyikiwa wakati tunapo ongea. Mara nyingi watu wanapouliza maswali magumu na ya kutisha tunachanganyi-kiwa na mara nyingi tunakosa la kusema. Kwa matokeo, tunajisikia wanyonge na kupungukiwa kwa majibu. Lakini

tunapoomba na kusoma neno la Mungu, Mungu atatupatia hekima ili tujuwe vile tutajibu.

**7.** Ni majaribu gani unayotarajia kukupata unapoamua kuwa Mkristo?

**8.** Tena, Petro anatufundisha kwa maarifa kwamba, *"Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mazuri, ikiwa ndio mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya"* (1 Petro 3: 17). Unaweza kumfurahisha kila mtu wakati wowote? Kama hapana, ni nani basi atakaye stahili umfurahishe, Mungu au binadamu? (Version: Swahili Union Version)

**9.** Mwisho, Petro anatukumbusha kuhusu Yesu, *"Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; Mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa"* (1 Petro 3: 18).

Tunapokumbuka mfano wa Yesu, tunapata nguvu. Alipatwa na majaribu mengi kwa niaba yetu, kwa hiyo tunastahili kuwa wavumilivu katika majaribu na mateso yanapotupata katika maisha yetu. Majaribio yako yatafananishwaje na ya Yesu? Yesu anajua fikira zetu wakati tunapopata majaribu kwa sababu ya hayo tunayopitia.

**Kwa sababu ya mateso na majaribu yatakayo kuja, tunahitaji kufikiria bila mzaha kama tunaweza kuvumilia na kusimama imara wakati wa majaribio. Tunahitaji kufanya haya kabla hatujakata shauri kuwa Wakristo.**

Vile vile tunahitaji kuelewa kwamba Mungu atatusaidia kusimama imara kupigana na chochote ambacho itakuja upande wetu na kutupatia tuzo kwa imani yetu. Haya maandiko yanatuhakikishia haya: Matayo 16:24-28; Matayo 19: 29, 30; Marko 10:28-31; Yohana 14: 1-4; Yohana 16: 33;

Warumi 8:38, 39; 1 Wakorintho 10: 11-13; 2 Petro 1:10, 11; 2: 9.

**10.** Vile tunavyotarajia mambo magumu yanayokuja hatuna budi kukumbuka ya kwamba tunapokuwa Wakristo tunastahili kujitoa sisi wenyewe katika mwili wa waamini kwa ushirika na uzima wa kiroho. Wahebrania 10: 24, 25 inatupatia nguvu yakufanya hivyo. Inasema, "Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tisiache kukusanyika pamoja, kama ilivyodesturi ya wengine; bali tuonyane; naa kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia." (Vile vile soma mistari hizi za maana kabisa: Matendo ya Mitume 2: 42- 47.)

**11.** Wahebrania 3: 12, 13 Inasema tunahitaji kutiana moyo sisi kwa sisi daima maadamu inaitwa leo, ili asipatikane kati yenu atakaye fanywa ngumu na dhambi.

**12.** Vile vile hatuna budi kujitoa nafsi zetu kukuwa na kuwa zaidi kama Kristo – 2 Petro 3: 17, 18. Petro anasema, *"Basi, wapenzi , mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha udhibiti wenu. Lakini kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye, sasa na hata milele! Amina."*

**13.** Bibilia inasema katika 2 Wakorintho 3: 18, *"Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha Utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho."*

**14.** Tunamtumaini Mungu atusaidie tuweze kubadilishwa kuanzia ndani hadi nje. Katika Matayo 23:25-26, Yesu aliwakemea viongozi wa dini kwa sababu hawajafanya hivyo.

Akawaambia, *"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyanganyi na kutokuwa na kiasi!. Ewe Farisayo kipofu safisha kwanza ndani ya kikombe,ili nje yake nayo ipate kuwa safi."*

**15.** Yesu anasema kilicho ndani ndicho cha maana zaidi. *"Kinachotoka ndani ya mtu ndicho kinachomtia najisi. Kwa maana kutoka ndani, katika moyo wa mtu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wizi, uuaji, uzinzi, uchoyo, udanganyifu, ufisadi, wivu, kashfa, kiburi na upumbavu. Maovu hayo yote yatoka ndani ya mtu nayo humtia mtu najisi"* (Marko 7:20-23).

Majibu kwenye nafasi wazi katika mawazo yanayo husu mambo magumu yanayokuja inaendelea:

# Baraka za Kufunga

Mungu aendelee kukubariki kadri unavyo mfuata Yesu. Kila siku akupatie nafasi ya kuwabariki wengine kama vile alivyokubariki. Akujaliye nia ya kushiriki njia ya wokovu pamoja na wengine. Uendelee kukua ndani ya Kristo na kutambua unyonge na kumtamani katika udhaifu wako. Ubadilishwe mara kwa mara kwa jinsi yake. Uwapende wengine kwa Roho wa Yesu. Usikate tamaa hata siku moja unaposuluhisha matatizo yako pamoja na Mungu. Usichoke kukazana katika maombi mpaka usikie amani kutoka kwa Mungu kuhusu mateso au mahitaji yako.

Nitaomba ili kila siku utafute amani, tafuta kwa bidii na amini kwamba kwa kupitia njia hii Mungu atakupatia furaha. Vile vile, nitaomba ili utambue kwamba nyakati nyingine Mungu anatufanya tukuwe kupitia majaribu, kutubariki, na kutuongoza kwa amani na furaha.

Kila wakati utazame wengine kupitia macho ya Yesu na kuwapenda katika pendo la kudumu na sio katika pendo la ubaguzi wa chuki.

Mungu aendelee kukupatia moyo wenye kupenda na lenye pendo la ujasiri kwa mataifa yote.

***"Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote"*** (2 Wakorintho 13: 14).